

**MWAMUHUDUMIA NANI?**

1. Malenga nina maswali, nayaleta kilingeni  
Yana husu serikali, na siasa za bungeni  
Askari tafadhali, na wanajeshi kambini  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
2. Jeshi ni la serikali, au raia nchini?  
Museme leo ukweli, munafanya kazi gani  
Raia wastahili, majibu yenu wapeni  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
3. Polisi wajibu swali, kazi yao hasa nini  
Kwa vikundi mbali mbali, kazi zenu zisemeni  
Musidai siri kali, ni wajibu mubaini  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
4. Kwa kero kula hatuli, bila hongo mkononi  
Usipotoa hulali, ole wako umbioni  
Utazona dalili, za kwenda korokoroni  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
5. Dhuluma hizi ni kweli, wazalendo matesoni  
Askari wahalali, watia watu tabuni  
Hizi zote ni dalili, raia hana thamani  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
6. Na wanasisia tuli, haya katu kuyalani  
Kazi zao udalali, misaada ya kigeni  
Wajikorombeze wali, na michuzi bakulini  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
7. Mwanasisia halali, siku za kura mbioni  
Ashindapo basi kweli, hawi tena masikini  
Ajabu mwaka wa pili, ndiye tajiri mjini  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
8. Mali ya uma kwa kweli, kinyang'anyiro jueni  
Huduma za serikali, walipao masikini  
Nyumba, magari ya ghali, wanasisia peponi  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
9. Wazalendo zao hali, wameachwa matopeni  
Wafanyakazi dhalili, chumo laisha jikoni  
Kwao mambo ni mawili, kula, kulipa madeni  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
10. Shule wamezibadili, walimu walipwa nini?  
Ukenda hospitali, mateso hutaamini  
Waziri hapo halali, enda nchi za kigeni  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
11. Aibu duara hili, raia kuwekwa ndani  
Dhuluma za serikali, polisi paka jeshini  
Hamuoni hii hali, YARABI aibu gani!  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
12. Mwenye pesa ni adili, ndiye mtu wa thamani  
Mwafanya nao shughuli, kupora mali nchini  
Mwatutia silisili, na bunduki mkononi  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
13. Shekhe atoe kauli, aseme msikitini  
Huu uizi wa mali, ukome serikalini  
Polisi na mbwa kali, ona cha mtema kuni  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili?
14. Tama nafunga kauli, tulidhanja zamani  
Utawala wetu kweli, utakuwa wa imani  
Hatukuona dalili, kwa haya hatukudhani  
Mwamuhudumia nani, kati ya hawa wawili.

*B. Mwamboga  
Holland  
April 08, 2003*